TANGAZO LA SERIKALI NA. 496 la tarehe 15/7/2022

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA YA 290

-------------

# SHERIA NDOGO

-------------

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (VITUO VYA MABASI NA MAEGESHO YA VYOMBO VYA MOTO) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO ZA MWAKA 2022

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Vituo vya Mabasi na Maegesho ya Vyombo vya Moto) za Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo za Mwaka 2022.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo:-

*"Ada na ushuru"* maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala wake kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

*"Afisa Mwidhiniwa"* Maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

*"Chombo cha Usafiri"* maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha Mtu, Watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa Wanyama, Mikokoteni na Baiskeli;

"*Halmashauri"* Maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo;

Sura ya 413

*"Kituo cha Mabasi"* maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kushusha abiria na mizigo ya Abiria;

*"Maegesho''* Sehemu yeyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha vyombo vya usafiri kwa muda;

*"Mkurugenzi"* maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo au Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"LATRA" Maana yake ni kama ilivyotafsiriwa na Sheria ya udhibiti wa vyombo vya

usafiri;

"Ushuru" maana yake ni tozo au malipo yatakayolipwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

## SEHEMU YA PILI
## VYOMBO VYA USAFIRI

Wajibu wa Halmashauri

4. Halmashauri ina wajibu wa kuweka utaratibu wa usimamizi na matumizi ya barabara, vituo vya mabasi na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya maegesho ya magari.

## SEHEMU YA TATU
## VITUO VYA MABASI.

Wajibu wa kuanzisha vituo vya mabasi

5.(1) Halmashauri itaanzisha vituo vya mabasi yanayofanya shughuli zake ndani ya eneo la Manispaa ya Ubungo, yanayotoka nje ya Halmashauri na yanayoingia ndani ya Halmashauri kwa ajili ya abiria na mizigo.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 5(1) cha Sheria Ndogo hizi mabasi yatajumuisha mabasi yaendayo mikoani na nje ya nchi pamoja na mabasi madogo ya abiria yanayofanya shughuli zake ndani ya Halmashauri maarufu kama daladala.

Wajibu wa kutumia vituo vya mabasi

6.(1) Ni wajibu wa kila mmiliki au msimamizi wa mabasi yatokayo na yaendayo mikoani na nchi jirani, kuingia katika eneo ambalo limetengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria na mizigo.

(2) Ni Marufuku kwa mtu yeyote, Mmiliki wa chombo cha usafiri au taasisi yoyote kuanzisha kituo cha mabasi, kushusha, kupakia abiria au

mizigo katika eneo ambalo halijatengwa au kutambuliwa kwa kupewa kibali na Halmashauri kwa ajili ya kituo cha mabasi.

(3) Isipokuwa kwa kibali maalum kutoka Halmashuri, mabasi yote yanatakiwa kuanza safari zake katika stendi iliyotengwa.

(4) Ni marufuku kampuni na wamiliki wa mabasi kuweka wapiga debe au mawakala katika maeneo yote yanayozunguka stendi za mabasi.

(5) Tiketi zote za wasafiri zitakatwa katika ofisi rasmi za mabasi zilizo ndani ya vituo vya mabasi au kwa njia ya kielektroniki.

(6) Tiketi zote zisizo za kieletroniki ambazo zimekatwa nje ya kituo cha mabasi zitachukuliwa kama batili na hazitatumika kama mbadala wa ushuru wa kuingia kituoni.

(7) Ni marufuku kufungua ofisi, kituo au kufanya biashara inayofanana na shughuli zinazofanywa katika kituo cha mabasi katika eneo lote la Halmashauri.

(8) Halmashauri itatoza ushuru kwa watumiaji wa Kituo cha mabasi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza ya Sheria Ndogo hizi.

Orodha ya Watumiaji wa kituo cha Mabasi

7. (1) Halmashauri itaweka utaratibu wa kuwatambua watumiaji wa vituo vya mabasi kwa mujibu wa vyama au vyombo vilivyosajiliwa na kutambulika na Sheria za Nchi na kuandikishwa na Halmashauri.

(2) Watumiaji wa vituo watalazimika kuvaa vitambulisho maalum vitakavyotolewa na Halmashauri wakati wote wawapo kituoni.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kupiga debe au kufanya kitendo chochote kinachopelekea abiria kutotumia huduma zinazotolewa na Halmashauri

*Tanagazo la serikali na. 496 (linaendelea)*

katika kituo cha mabasi.

(4) Ni marufuku kwa Watumiaji wa vituo vya mabasi kutumia lugha ya matusi na kubughudhi abiria kunakopelekea kuhatarisha amani na utulivu ndani na nje ya vituo vya mabasi.

(5) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote atakayekwenda kinyume na kifungu cha 7 cha Sheria ndogo hizi na endapo atapatikana na hatia atatozwa faini ya shilingi Elfu Hamsini (50,000/=) au kutumikia kifungo kisichozidi Miezi kumi na Mbili jela au vyote kwa pamoja.

Ushuru wa maegesho kwenye vituo vya mabasi.

8. Halmashauri itatoza ushuru wa vyombo vya usafiri kwa ajili ya maegesho katika maeneo yaliyotengwa, kuingia katika kituo cha mabasi, kulaza gari na kuegesha gari ndani ya kituo cha mabasi kama ilivyoainishwa katika jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

Mabango ya matangazo ya biashara

9. Halmashauri itatoza kodi ya pango la eneo la kuweka bango la matangazo katika eneo lolote ndani ya vituo vya mabasi kwa mujibu wa viwango vitakavyoelekezwa na Halmashauri kulingana na vipimo vya bango husika.

Usafi wa Mazingira

10 (1) Ni wajibu wa kila mtumiaji wa kituo cha mabasi kuhakikisha kuwa anatunza mazingira kwa kutotupa ovyo taka za aina yoyote au kutiririsha maji katika eneo la kituo cha mabasi.

(2) Kila mmiliki wa chombo cha usafiri atahakikisha kuwa anaweka chombo cha kutupia na kutunza taka ndani ya chombo cha usafiri na kutupa taka hizo katika maeneo maalum ndani ya kituo cha mabasi.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa taka ovyo, kumwaga au kutiririsha maji ovyo, kuosha vyombo vya usafiri katika vituo vya mabasi isipokuwa katika eneo lililotengwa kwa ajili hiyo.

(4) Ni marufuku kwa watumiaji wa vituo vya mabasi kujisaidia kwenye sehemu isiyo rasmi.

(5) Matumizi ya vyoo na bafu kwenye vituo vya mabasi yatalipiwa kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi.

SEHEMU YA NNE
MAEGESHO YA MAGARI NDANI YA HALMASHAURI

Maeneo ya Maegesho Nje ya vituo vya Mabasi.

11 (1) Halmashauri itatenga maeneo kwa ajili ya maegesho ya magari binafsi, teksi na magari ya mazigo au vyombo vingine vya usafiri.

(2) Halmashauri itaweka alama au michoro maalum itakayoonesha maeneo ya maegesho au namna yoyote ile itakayoashiria eneo la maegesho ya magari au chombo kingine cha usafiri;

(3) Mtu yeyote, Kampuni au Shirika au Kikundi ambacho kitanzisha eneo au maeneo kwa ajili ya maegesho kitapaswa kuwa na kibali kutoka Halmashauri na kitapaswa kulipia maegesho hayo kwa mujibu wa makubaliano kati yake na Halmashauri.

(4) Maeneo ya maegesho yatafunguliwa kuanzia saa moja na dakika thelathini asubuhi (1:30) hadi saa kumi na moja jioni (11.00) katika maeneo ya kawaida.

(5) Bila kuathiti masharti ya kifungu kidogo cha 4 cha sheria ndogo hizi, maegesho ya magari makubwa ya mizigo yatakuwa kwa masaa

ishirini na nne.

Ushuru wa maegesho

12 (1) Halmashauri itatoza ushuru wa maegesho katika maeneo inayomiliki kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa katika Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hii.

(2) Halmashauri inaweza kutoa kibali kwa ajili ya maegesho katika maeneo maalum ***"Reserved area"*** endapo Mwombaji atalipa Ushuru wa maegesho kwa kipindi cha kuanzia wiki moja.

(3) Halmashauri itatoa stakabadhi ya kielektroniki kuthibitisha malipo ya ushuru wa maegesho kwa mmiliki au msimamizi wa chombo cha usafiri kulingana na muda alioutumia kuegesha chombo chake cha usafiri.

(4) Mtu yeyote atakayelipia ushuru wa maegesho kwa jumla ya gharama za siku, wiki au mwezi kwa mkupuo atapewa kibali maalum kitakachomruhusu kuegesha chombo cha usafiri katika eneo lolote lililotengwa na Halmashauri kwa maegesho bila malipo.

Maegesho yasiyo rasmi (Wrong parking)

13 (1) Ni marufuku kuegesha gari au chombo chochote cha usafiri katika maeneo yasiyotengwa kwa ajili ya maegesho, au kuegesha kwa namna isiyoruhusiwa.

(2) Halmashauri itakikokota au itakizuia kwa kukifunga vifaa maalum chombo cha usafiri kilichoegeshwa isivyoruhusiwa au kilichoegeshwa katika eneo lisiloruhusiwa na kumtaka mmiliki kulipa faini ya papo kwa papo kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na Sheria Ndogo hizi.

*Tanagazo la serikali na. 496 (linaendelea)*

Gharama za Uondoaji na Uvutaji wa magari

14. (1) Halmashauri au Wakala atatoza gharama ya uvutaji, utunzaji pamoja na gharama zingine zitakazojitokeza wakati wa kukamata chombo cha usafiri kilichoegeshwa vibaya au kinyume cha matakwa ya Sheria Ndogo hizi.

(2) Gharama za uondoaji na uvutaji zitakuwa ni kama zilivyoainishwa kwenye Jedwali la Tano la Sheria Ndogo hizi.

(3) Pale ambapo chombo cha usafiri hakitachukuliwa kwa zaidi ya mwezi mmoja Halmashauri itakiuza kwa njia ya mnada wa hadhara au kukitaifisha baada ya kupata idhini ya mahakama.

(4) Halmashauri itatumia mapato yaliyopatikana katika kifungu kidogo cha (3) kulipia gharama ilizotumia na kiasi kilichobakia kitarejeshwa kwa mmiliki.

Msamaha wa kulipa ushuru wa Maegesho

15. (1) Halmashauri haitatoza ushuru wa maegesho kwa vyombo vya usafiri vifuatavyo; -

(a) Magari ya Serikali
(b) Magari ya Kibalozi
(c) Magari yaliyoegeshwa katika sehemu za Ibada *(muda wa ibada)*
(d) Magari yaliyo na vibali maalumu kutoka Halmashauri
(e) Magari yaliyoegesha katika maeneo ya maegesho wakati wa shughuli maalum za kitaifa.

Uteuzi wa wakala

16. Halmashauri itakuwa na Mamlaka ya kuteua Taasisi au Kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria kukusanya ushuru wa stendi au maegesho kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

*Tanagazo la serikali na. 496 (linaendelea)*

Wajibu wa wakala

17. Wakala aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 16 cha sheria ndogo hizi, atakuwa na wajibu wa-

(a) Kukusanya na kupokea ushuru wa stendi au maegesho kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

(b) Wakala atakusanya ushuru wa stendi au maegesho kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Makosa na Adhabu

18. Ni kosa kwa Mtu yeyote endapo;

(a) Atamzuia Afisa Mwidhiniwa au Wakala wa Halmashauri kutekeleza majukumu yake ya kusimamia Sheria Ndogo hizi.

(b) Ataharibu kwa namna yoyote miundo mbinu ya barabara, vifaa, kamera za usalama au taa za barabarani katika maeneo ya maegesho na vituo vya mabasi.

(c) Atajaribu au atakusanya Ada au Ushuru bila idhini ya Halmashauri.

(d) Ataegesha chombo cha usafiri katika maeneo yasiyo rasmi kwa maegesho *(wrong parking);*

(e) Atakataa, atashindwa au atashawishi mtu yeyote kutolipa viwango vya ada na ushuru vilivyoainishwa na Sheria Ndogo hizi.

(f) Ataingia katika kituo vya mabasi pasipo kulipia ushuru husika.

(g) Atalaza chombo cha usafiri, ataosha, atatengeneza, au atafanya shughuli yoyote isiyoruhusiwa ndani Kituo cha mabasi.

(h) Atachafua mazingira kwa kutupa taka za aina yoyote ndani ya kituo cha mabasi au atatupa taka kutoka kwenye chombo cha usafiri;

Atatenda jambo lolote ambalo ni kinyume cha Sheria Ndogo hizi

Adhabu

19. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na iwapo atapatikana na hatia na kama hakuna adhabu maalumu iliyoainishwa katika kifungu kilichokiukwa atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi Milioni Moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua Miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi Ishirini na Nne au vyote kwa pamoja faini na kifungo;

Kufifilisha kosa

20 Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa endapo
Mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewe na kukubali kulipa faini ya kiasi cha Shilingi Laki Mbili (200,000/=) na kujaza fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Sita pamoja na kulipa kiasi cha ushuru anaodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetungwa Chini ya Kifungu cha 6(8))*

USHURU WA KUINGIA STENDI YA MABASI.

| Na. | Aina ya Chombo | Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Basi Dogo la abiria kati ya 1 - 20 | 2,000 kila linapoingia |
| 2. | Basi kubwa la abiria kati ya 20 - 28 | 5,000 kila linapoingia |
| 3. | Basi kubwa la abiria zaidi ya 28 | 10,000 kila linapoingia |
| 4. | Gari Dogo (Taxi Cab) | 1,000 kila linapoingia |
| 5. | Gari Dogo (Binafsi) | 1,000 kila linapoingia |
| 6. | Magari ya Mizigo (Pick-up) | 4,000 kila linapoingia |
| 7. | Trucks na Trailers zaidi ya tani 3 | 5,000 kila linapoingia |
| 8. | Trucks na Trailers tani 3 na zaidi | 10,000 kila linapoingia |
| 9. | Pikipiki Miguu Mitatu/guta | 2,500 kila inapoingia |
| 10. | Pikipiki | 500 kila linapoingia |
| 11. | Magari mengine | 1,000 kila linapoingia |
| 12. | Baiskeli | 500 kila inapoingia |
| 13. | Ada ya Kuingia mtu mmoja | 500 kila anapoingia |
| 14. | Kufunga magari | 30,000 kwa gari |

JEDWALI LA PILI

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 8)*

USHURU WA KULAZA GARI NDANI YA STENDI YA MABASI KWA SIKU

Sehemu A.

| *Na.* | *Aina ya Chombo* | *Ushuru wa kulaza Gari* |
|---|---|---|
| 1. | Gari Dogo la abiria kati ya 1-20 | 3,000 |
| 2. | Gari kubwa la abiria zaidi ya 20-28 | 4,000 |
| 3. | Gari kubwa la abiria zaidi ya 28 | 5,000 |
| 4. | Gari Dogo (Taxi Cab) | 3,000 |
| 5. | Gari Dogo (Binafsi) | 3,000 |
| 6. | Trucks na Trailers zaidi ya tani 3 | 5000 |
| 7. | Trucks na Trailers tani 3 na zaidi | 10,000 |
| 8. | Magari ya Mizigo (Pick-up) | 3,000 |
| 9. | Magari mengine | 3,000 |
| 10. | Pikipiki ya miguu mitatu/guta | 2,000 |

USHURU WA MAEGESHO KATIKA VITUO VIKUU VYA MABASI

Sehemu B

| *Na.* | *Aina ya Chombo cha usafiri* | *Ushuru wa Siku* |
|---|---|---|
| 1. | Gari Dogo (Taxi Cab) ndani ya kituo | 4,000 kwa siku |
| 2. | Gari Dogo (Taxi Cab) nje ya kituo | 3,000 kwa siku |
| 3. | Magari ya Mizigo (Pick-up) ndani ya kituo | 4,000 kwa siku |
| 4. | Trucks na Trailers zaidi ya tani 3 | 5,000 kwa siku |
| 5. | Trucks na Trailers tani 3 na zaidi | 10,000 kwa siku |
| 6. | Magari mengine ndani ya kituo | 3,000 kwa siku |
| 7. | Pikipiki ya miguu mitatu/guta | 2,000 kwa siku |
| 8. | Pikipiki | 1,000 kwa siku |

USHURU WA MAEGESHO KATIKA VITUO VIKUU VYA MABASI

Sehemu C

| *Na.* | *Aina ya Chombo cha usafiri* | *Ushuru wa Saa* |
|---|---|---|
| 1. | Gari Dogo (Taxi Cab) ndani ya kituo | 1,000 kwa saa |
| 2. | Gari Dogo (Taxi Cab) nje ya kituo | 1,000 kwa saa |
| 3. | Magari ya Mizigo (Pick-up) ndani ya kituo | 1,500 kwa saa |
| 4. | Trucks na Trailers zaidi ya tani 3 | 2,000 kwa saa |
| 5. | Trucks na Trailers tani 3 na zaidi | 3,000 kwa saa |
| 6. | Magari mengine ndani ya kituo | 1,000 kwa saa |
| 7. | Pikipiki ya miguu mitatu/guta | 1,000 kwa saa |
| 8. | Pikipiki | 500 kwa saa |

JEDWALI LA TATU

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 10(5))*

**USHURU WA CHOO NA BAFU KITUO CHA BASI.**

| Na. | Aina ya huduma | Muda |
|---|---|---|
| 1. | Matumizi ya Choo | 500 kwa huduma. |
| 2. | Matumizi ya bafu | 1000 kwa huduma. |

JEDWALI LA NNE

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 12(1))*

USHURU WA MAEGESHO KWENYE MAENEO MENGINE YANAYOMILIKIWA NA HALMASHAURI.

| Aina ya Chombo cha usafiri | Ushuru wa saa |
|---|---|
| Gari Dogo | 1,000 |
| Magari ya Mizigo (Pick-up) | 1,000 |
| Trucks na Trailers zaidi ya tani 3 | 1,500 |
| Trucks na Trailers tani 3 na zaidi | 2,000 |
| Magari mengine | 1,000 |
| Pikipiki ya miguu mitatu/guta | 5,00 |
| Pikipiki | 5,00 |

*Tanagazo la serikali na. 496 (linaendelea)*

JEDWALI LA TAN0

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 14(2))*

GHARAMA ZA UONDOAJI NA UVUTAJI

| | |
|---|---|
| Gharama ya uondoaji gari | 100,000/= |
| Ufungaji(Clamping Charge) | 80,000/= |

JEDWALI LA SITA

*(Chini ya kifungu cha 20)*

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi …………………… nakiri mbele ya …………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashuri ya Manispaa ya ubungo, kwamba mnamo tarehe …… ya Mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za Halmashuri ya Manispaa ya Ubungo (Vituo vya Mabasi na Maegesho ya Vyombo vya Moto) za Mwaka 2022.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi, Niko tayari kulipa faini niliyopangiwa kuilipa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi………… Mwaka ………………….

*Jina*……………………………….. *Saini*…………………………

Mbele ya :

Jina: ……………………………………………

Cheo: ………………………………………….

Saini: …………………………………………..

Nembo na muhuri wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuata Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika mnamo tarehe 13 Mwezi Agosti, 2022.

BEATRICE R. DOMINIC,
*Mkurugenzi wa Halmashauri*
*ya Manispaa Ubungo*

JAFFARY JUMA NYAIGESHA
*Mstahiki Meya,*
*Halmashauri ya Manispaa Ubungo*

L.S

NAKUBALI

DODOMA
29 Juni, 2022

INNOCENT L. BASHUNGWA
*Waziri wa Nchi- or -Tamisemi*